BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA WA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Nane – Tarehe 02 Disemba, 2016.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo, la 2012.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam.12 ya 2004 na Kutunga Sheria inayoweka Masharti Bora Yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo Yanayohusiana na Hayo

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na Kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo Yanayohusiana na Hayo

Wizara ya Afya:

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo, la 2012.

II. MASWALI:

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko:

142. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwa kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko mnamo mwezi wa Agosti 2016 wameanzisha ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi "**Pre- export Verification of Conformity" (PVoC).**

a) Je, ni changamoto gani zilizojitokeza tokea kuanza kwa ukaguzi huo.

b) Wizara imechukua hatua gani kutatua changamoto hizo.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

144. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa Waandishi wa Habari za Mawio wanalipwa kulingana na habari wanazopeleka, lakini malipo hayo ni madogo kulingana na ukubwa na ugumu wa kuzipata habari zenyewe, wakati mwingine huzipata habari hizo vijijini.

Je, ni lini Wizara itawaongezea posho waandishi wa habari za mawio angalau warejeshe nauli zao wanazotumia wakiwa katika kazi.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira :

56. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Katika Shehia ya Uroa kuna Hoteli inayoitwa Samaki Lodge iliyoongeza eneo lake kuelekea ufukweni kinyume na utaratibu. Ujenzi huo umechafua sana mazingira kwa kuzidisha kasi ya maji wakati yanapojaa na kupelekea kufukuliwa kwa makaburi na maji kuzidi sana kuelekea nchi kavu.

Ujenzi huo pia unaikosesha sana Serikali mapato kwani eneo hilo liliozidishwa halilipiwi kodi ya namna yoyote ile. Na hatua mbali mbali zimechukuliwa na Serikali ya Mkoa, Mamlaka ya Kuhifadhi Mazingira Zanzibar, Idara ya Mazingira pamoja na Serikali Kuu ili kuliondoa eneo hilo lililozidishwa lakini bado hazijazaa matunda na athari zake zinaendelea kuwepo.

Je, Serikali inachukuwa hatua gani zaidi kuhakikisha kuwa hatua za kisheria zinachukuliwa kudhibiti hali hiyo inayoiathiri sana jamii na Serikali kwa jumla.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

106. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuna walimu ambao walisimamishwa kazi kwa tuhuma ya vyeti vyao kuwa feki lakini baada ya Serikali kufuatilia ilionekana ni vyeti halali.

Je, haki yao ambayo hawakupewa Serikali inawafikiria vipi. Hasa kwa baadhi yao ambao wameshafariki na wameacha warithi wao.

111. MHESHIMIWA VIWE KHAMIS ABDALLA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mhe. Waziri, kwa kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna changamoto kubwa ya uhaba wa walimu wa masomo ya Art na Sayansi, na hivyo hupelekea walimu wa masomo ya Art kusomesha masomo ya Sayansi bila ya kuwa na utaalamu huo.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako inalijuwa hilo na kama inajuwa ni hatua gani ambazo mmeanza kuzichukuwa ili kuweza kutatua changamoto hizo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

70. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Naipongeza sana Wizara ya Kilimo kwa kupitia mpango wake wa Mivarf kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ujenzi wa barabara za vijijini kwa kiwango cha kifusi zenye urefu wa km 82.7 huko Pemba. Kwa kuwa barabara hizi zimeweza kuchangia shughuli nyingi za ustawi wa kiuchumi na kijamii zikiwemo kilimo na huduma nyengine za kijamii.

Je, ni lini barabara hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami ikizingatiwa kuwa kubaki katika kiwango cha kifusi zitaendelea kuharibika.

139. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Kwa kuwa Serikali iliweka utaratibu mzuri wa matumizi ya gari za Serikali hasa nyakati za usiku kwa kuomba kibali maalum kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Je, utaratibu huu umeishia wapi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo, la 2012.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Nembo Nam. 1 ya 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam.12 ya 2004 na Kutunga Sheria inayoweka Masharti Bora Yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016 na Mambo Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya 1992 na Kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na Mambo Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Wizara ya Afya:

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006 – Kusomwa kwa Mara ya Kwanza.

Zanzibar,
02 Disemba, 2016.

(Amour M. Amour)
KNY. KATIBU